


Halo
kutoka Jamhuri ya
Demokrasia
ya Kongo!



D. R. Congo
iko Afrika ya kati.
Takriban watu
milioni 80
wanaishi huko.

**Habari, Sisi
ni Margo na
Paolo!**



**Tunatembelea
Jamhuri ya
Demokrasia ya
Kongo, au D. R.
Congo.**



Katika D. R. Congo, watu wengi wanazungumza Kifaransa kanisani. Hiyo ndiyo lugha rasmi ya nchi. Lakini kuna lugha zingine takriban 250 zinazozungumzwa huko D. R. Congo!



Wamisionari kutoka kanisa letu walianza kufundisha watu katika D. R. Congo mnamo 1986. Sasa takriban watu 60,000 huko ni waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.



Sehemu kubwa ya D. R. Congo imefunikwa na misitu ya mvua. Ni nyumbani kwa wanyama wa kuvutia wa aina mbalimbali, kama vile tembo, sokwe, na faru. Mnyama huyu anaitwa Okapi.

D. R. Congo inajulikana kwa utamaduni wake mzuri wa sanaa, ikijumuisha sanamu za mbao, vikapu vya kusukwa, na barakoa.



Mwaka huu, D. R. Congo ilipata hekalu lake la kwanza! Waumini wa Kanisa huko wanafurahi kuwa na hekalu katika nchi yao.

**Asante kwa kutalii
D. R. Congo pamoja
nasi. Tutaonana wakati
mwingine!**

Kutana na baadhi ya rafiki zetu kutoka D. R. Congo!



"Jumapili moja, kulikuwa na wanajeshi kila mahali na wazazi wangu walisema ilikuwa vigumu kwenda kanisani. Niliwaambia wazazi wangu kwamba tulipaswa kuhudhuria angalau mkutano wa sakramenti. Kwa pamoja tulionyesha imani na kwenda kanisani kuitakasa siku ya Bwana."

Prodi K., miaka 7, Kinshasa, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo



"Ninapenda kuwasaidia wengine. Siku moja katika darasa langu, mtoto alikuwa na huzuni kwa sababu wakati wa mapumziko hakuwa na chochote cha kula. Nilimwendea na kushiriki naye kile nilichobeba kwa ajili ya kula."

Célia Tshidibi K., miaka 5, Kinshasa, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo

Je, wewe unatoka D. R. Congo? Tuandikie! Tungependa kusikia kutoka kwako. Ona ukurasa wa R24.